JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA

MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BIMA TANZANIA

TAARIFA YA UTENDAJI WA SOKO LA BIMA KWA KIPINDI CHA MIAKA MINNE (4) KUANZIA MWAKA 2021 HADI 2024

IMEWASILISHWA NA:

DKT. BAGHAYO A. SAQWARE
KAMISHNA WA BIMA
AGOSTI, 20

1. UTANGULIZI

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) ni Taasisi ya Umma iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Bima Sura ya 394 kwa lengo la kuratibu usimamizi na maendeleo ya soko la bima ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kutokana na umuhimu wa bima kwa wananchi, Mamlaka kwa kushirikiana na wadau wake imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali yenye lengo la kuhakikisha kuwa huduma bora za bima zinawafikia wananchi wote kwa gharama nafuu.

1.2 MAJUKUMU YA MAMLAKA

Majukumu ya Mamlaka yamegawanyika katika maeneo makubwa matatu ambayo ni majukumu ya Kisheria, Majukumu ya Kiutawala na Majukumu yanayotokana na maagizo ya Serikali kama ifuatavyo:-

1.2.1 Majukumu ya Kisheria

Haya ni majukumu yaliyoainishwa katika Sheria ya Bima Sura ya 394 ambayo ni pamoja na kusajili watoa huduma za bima na kutoa leseni, Kuandaa na kutoa Kanuni na Miongozo ya Usimamizi wa Soko la Bima, Kulinda haki za wakata bima nchini, Kuendeleza soko la bima kwa kuhakikisha linakuwa salama, endelevu na stahimilivu; na kuishauri Serikali kuhusu masuala ya kisera ya Bima nchini.

1.2.2 Majukumu ya Kiutawala

Majukumu haya yanahusu **Maagizo mbalimbali** yanayotolewa na **Bodi** kulingana na mahitaji ya wadau ikiwemo kupendekeza marekebisho ya Sheria, Kanuni na Miongozo ili kuboresha utendaji wa shughuli za Mamlaka na kutoa maagizo kwa Menejimenti kuhusu Sera na Miongozo mbalimbali.

1.2.3 Maagizo ya Serikali

Maagizo yanayotokana na utekelezaji wa Sera za Serikali mfano utawala bora na uwajibikaji na ahadi za Serikali Bungeni ikiwemo maagizo kutoka kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya

Hesabu za Serikali (PAC) na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC).

2. OFISI ZA MAMLAKA

Katika kutekeleza majukumu na kusogeza huduma kwa wananchi, hadi sasa Mamlaka imefungua ofisi kuu tatu ambazo ni Makao Makuu Dodoma, Ofisi ya Zanzibar, Ofisi ya Dar es Salaam pamoja na Ofisi Kumi (10) za Kanda.

Jedwali Na 1: Mchanganuo wa Ofisi za Kanda za Mamlaka

Na	Kanda	Mikoa husika	Ofisi ilipo
1	Kanda ya Nyanda za Juu Kusini	Mbeya, Njombe & Songwe	Mbeya
2	Kanda ya Kaskazini	Arusha, Kilimanjaro & Tanga	Arusha
3	Kanda ya Ziwa	Mwanza, Mara, Kagera, Simiyu & Geita	Mwanza
4	Kanda ya Mashariki	Dar es Salaam, Pwani, & Morogoro	Dar es Salaam
5	Kanda ya Kati	Dodoma, Manyara & Iringa	Dodoma
6	Kanda ya Magharibi	Tabora, Shinyanga & Singida	Tabora
7	Kanda ya Kusini	Mtwara, Lindi & Ruvuma	Lindi
8	Kanda ya Ziwa Tanganyika	Katavi, Rukwa & Kigoma	Katavi
9	Kanda ya Unguja	Kaskazini Unguja, Kusini Unguja & Mjini Magharibi	Mjini Magharibi
10	Kanda ya Pemba	Kaskazini Pemba & Kusini Pemba	Kusini Pemba - Chakechake

3. HALI YA UTENDAJI WA SOKO LA BIMA KWA MIAKA MINNE YA UONGOZI WA DKT. SAMIA SULUHU HASSAN

Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu,** imeendelea kuweka mazingira rafiki ya ufanyaji biashara katika sekta mbalimbali nchini ikiwemo sekta ya bima nchini. Kupitia sera madhubuti na mazingira wezeshi ya uwekezaji, sekta hii muhimu kwa ustawi wa jamii na uchumi wa taifa imeendelea kukua kwa kasi, kuongeza upatikanaji wa huduma za bima kwa wananchi, na kuongeza uwezo wa kukabili majanga mbalimbali yanayoweza kuathiri maisha na uchumi wa nchi.

Watanzania wengi zaidi sasa wananufaika na huduma za bima, huku fidia zikitolewa kwa walioathirika na majanga mbalimbali, hivyo kusaidia kulinda maisha na mali zao. Mafanikio haya yametokana na juhudi mahususi za Serikali ya Awamu ya Sita katika kuweka mikakati na kuchukua hatua mbalimbali za kisera, kisheria na kiutendaji kuimarisha sekta hii.

3.1 Maswala yaliyotekelezwa na Serikali ya Awamu ya Sita katika Sekta ya Bima

Katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa **Mhe Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ya Awamu ya Sita imetekeleza mambo mengi muhimu ambayo yamewezesha ukuaji na uimarishaji wa sekta ya bima nchini. Hatua hizo zilizochukuliwa na Serikali zimeongeza upatikanaji wa huduma bora za bima kwa wananchi, kuvutia wawekezaji wapya, na kuimarisha mifumo ya usimamizi wa Sekta ya Bima . Baadhi ya hatua hizo muhimu ni pamoja na:-

a. **Kuteua Bodi ya Taifa ya Bima**: Serikali ya Awamu ya Sita iliteua wajumbe wa Bodi ya Taifa ya Bima, wakiwemo wataalamu wenye uzoefu na uelewa mpana wa sekta ya bima. **Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan** alimteua Mwenyekiti wa Bodi ambaye ameendelea kutoa dira, ushauri na miongozo muhimu kwa ajili ya maendeleo ya Sekta ya Bima nchin. Bodi ya Bima imekuwa kiungo muhimu katika kusimamia utekelezaji wa masuala ya Kisera na mikakati mbalimbali ya kukuza soko la bima nchini.

b. **Matamasha ya kibiashara:** Serikali, kwa kushirikiana na wadau wa sekta binafsi, imeendelea kuratibu na kushiriki kwenye matamasha ya kibiashara ya bima ndani na nje ya nchi. Matamasha hayo yamelenga kuhamasisha Umma kuhusu dhana na umuhimu wa bima, kujenga mahusiano ya kibiashara, na kufungua fursa mpya za uwekezaji katika Sekta ya Bima.

c. **Kuvutia wawekezaji:** Kufuatia maboresho ya kisera na kisheria, idadi ya kampuni za bima na kampuni za bima mtawanyo (reinsurance) zimeongezeka nchini. Wawekezaji wapya wamevutiwa na mazingira bora ya ufanyaji wa biashara ya bima na uthabiti wa kiuchumi.

d. **Kutungwa kwa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote na Kanuni zake:** Miongoni mwa mafanikio makubwa ya Serikali ya Awamu ya Sita ni kutungwa kwa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote mwaka 2023 na Kanuni zake. Sheria hiyo ilipitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kusainiwa na Mheshimiwa Rais, ikiwa ni hatua ya kihistoria inayolenga kuhakikisha Watanzania wote wanapata huduma bora za afya kupitia mfumo wa bima. Aidha, mwaka 2024, Serikali kupitia Wizara ya Afya iliandaa na kupitisha Kanuni za Bima ya Afya kwa Wote ili kuwezesha utekelezaji wa Sheria hiyo muhimu. Kanuni hizo zimeweka misingi ya utekelezaji, usimamizi, na ushirikishwaji wa wadau katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya bima ya afya kwa kila Mtanzania.

e. **Maboresho ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2022:** Serikali ya Awamu ya Sita imefanya maboresho katika Sheria ya Fedha ya mwaka 2022 ambayo imeongeza wigo wa bima za lazima katika maeneo muhimu ikiwemo bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi (imported goods) kuwa na bima za kampuni za ndani, majengo ya Umma na biashara kuwa na bima, vivuko na pantoni kuwa na bima. Aidha, Serikali imendelea kuhakikisha kuwa miradi yake mikubwa ya kimkakati inayotekelezwa nchini, ikiwemo ya miundombinu, inakuwa na kinga ya bima kutoka kwa kampuni za bima za ndani ili kulinda mali na uwekezaji unaofanywa na Serikali. Hatua hii inalinda uwekezaji wa Taifa na kuhakikisha kuna uendelevu wa miradi hiyo muhimu.

f. **Kuanzishwa kwa Konsortia ya Bima ya Kilimo:** Kupitia ushirikiano na wadau, Serikali imeanzisha Konsotia ya Bima ya Kilimo kwa lengo la kuwahudumia wakulima, kupunguza athari za majanga ya asili, na kuongeza tija katika sekta ya kilimo. Hii ni sehemu ya juhudi za Serikali za kuhakikisha kuwa wakulima wanakuwa na uhakika wa kipato hata wanapokumbwa na majanga.

g. **Kuanzishwa kwa Konsotia ya mafuta na gesi:** Sekta ya mafuta na gesi, ikiwa ni eneo la kimkakati kwa uchumi wa nchi, imenufaika na uanzishwaji wa konsotia maalum ya bima inayolenga kusimamia hatari na kulinda uwekezaji katika maeneo haya muhimu kwa uchumi wa nchi.

h. **Kuimarishwa kwa Mifumo ya TEHAMA :** Kwa kutekeleza maagizo ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ya Awamu ya Sita imefanikisha hatua kubwa ya kuunganisha mifumo ya TEHAMA ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) na taasisi nyingine muhimu za Serikali. Miongoni mwa taasisi zilizounganishwa ni pamoja na Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), Mamlaka ya Usafiri Baharini (TASAC), Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), na taasisi nyinginezo.

   Muunganiko huu wa mifumo umesaidia kuongeza uwazi, ufanisi wa usimamizi wa taarifa, urahisi wa kufuatilia mwenendo wa sekta ya bima, na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi. Hatua hii ni ya kimkakati katika kujenga sekta ya bima inayozingatia matumizi ya teknolojia na inayoshirikiana kikamilifu na mifumo mingine ya kitaifa kwa maendeleo endelevu.

i. **Kuimarisha matumizi ya kidijitali:** Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya uongozi wa Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeweka mazingira wezeshi yanayochochea matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma kwa Umma. Kupitia mazingira ya biashara yaliyoboreshwa, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) imetengeneza mfumo wa kidijitali wa usajili unaowawezesha wananchi na wawekezaji wanaotaka kutoa huduma za bima nchini kuweza kujisajili mahali popote walipo.

   Kupitia mfumo huo, waombaji wa usajili hawalazimiki kufika katika ofisi za TIRA, bali wanaweza kutuma maombi yao mtandaoni, kufuatilia hatua kwa hatua, na hatimaye kupata cheti cha usajili kwa njia ya kidijitali. Hatua hii imeongeza uwazi, kuondoa urasimu, kupunguza gharama na muda wa usajili, na kuimarisha utoaji wa huduma kwa kasi na ubora unaotarajiwa katika zama za kidijitali.

j. **Uanzishwaji wa Takaful:** Serikali ya Awamu ya Sita imewezesha uanzishwaji wa huduma ya bima ya Takaful ili kuhakikisha kuwa wananchi wanaofuata misingi ya Kiislamu nao wanapata huduma za bima zinazozingatia imani zao. Hatua hii imepanua

wigo wa ujumuishaji wa kifedha katika jamii kwa kuwa aina hiyo ya bima inawezesha makundi mbalimbali ya wananchi kutumia aina hiyo ya bima kulinda mali zao.

4. UTENDAJI WA SOKO LA BIMA KUANZIA MWAKA 2021 HADI 2024

Kutokana na utekelezaji wa Sera nzuri chini ya uongozi mahiri wa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu**, Sekta ya Bima imeendelea kuimarika na kupata mafanikio makubwa. Mafanikio haya yanadhihirika katika muhtasari wa takwimu za utendaji wa soko la bima kwa kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka 2021 hadi 2024 kama ifuatavyo:-

4.1 Watoa huduma za bima

Idadi ya watoa huduma za bima imeongezeka kutoka 993 mwaka 2021 hadi kufikia 2,425 Juni 2025, sawa na ongezeko la jumla la asilimia 144.2. Ongezeko hilo ni sawa na wastani wa asilimia 22.1 kwa mwaka. Aidha, katika kipindi hicho, Mamlaka imeongeza aina mpya ya watoa huduma ikiwa ni pamoja na watoa huduma za afya (HSPs), warekebishaji na watengenezaji magari (ARMs) na Watoa Huduma Kidijitali. Vilevile, kampuni za bima mtawanyo nchini zimeongezeka kutoka kampuni moja (1) mwaka 2021 hadi kampuni nne (4) mwaka 2025;

Jedwali Na. 2: Usajili wa watoa huduma za bima hadi kufikia tarehe 30 Juni 2025

Watoa huduma	2021	30 Juni 2025
Kampuni za Bima Mtawanyo	1	4
Kampuni za Bima	32	35
Skimu za Bima ya Afya ya Umma	0	1
Skimu za Bima ya Afya ya Binafsi	0	1
Washauri wa Bima	82	146
Mawakala wa Bima	789	1,419
Washauri wa Bima Mtawanyo	4	11
Benkiwakala	23	35
Kampuni za Takwimu Bima	4	6
Wakadiriaji Hasara	50	68

Wachunguzi binafsi	4	7
Wauza Bima Kidijitali	4	17
Kampuni ya Usimamizi wa Amana na Mifuko ya Pensheni	0	1
Maafisa wauza bima (SFEs)	0	280
Watoa huduma za afya (HSPs)	0	154
Watengenezaji na watunza magari (ARMs)	0	239
Wakaguzi wa nje wanaohuduma sekta ya Bima	0	1
Total	**993**	**2,425**

4.2 Wanufaika wa Huduma za Bima

Wanufaika wa huduma za bima nchini wameongezeka kutoka milioni 14.2 mwaka 2021 hadi kufikia milioni 25.9 mwaka 2024, sawa na jumla ya ongezeko la asilimia 82.4 katika kipindi cha miaka minne, ikiwa ni wastani wa ongezeko la asilimia 22.2 kwa mwaka;

4.3 Ajira rasmi katika soko la bima

Ajira rasmi katika soko la bima zimeongezeka kutoka wafanyakazi 3,527 mwaka 2021 hadi kufikia wafanyakazi 6,916 tarehe 30 Juni 2025 sawa na ongezeko la asilimia 96.1. Ongezeko hilo ni sawa na wastani wa ongezeko la asilimia 18.3 kwa mwaka;

4.4 Mali na Mitaji Katika Soko la Bima

4.4.1 Mali za Bima

Thamani ya mali katika soko la bima imeongezeka kutoka shilingi trilioni 1.277 mwaka 2021 hadi kufikia shilingi trilioni 2.340 mwaka 2024, sawa na jumla ya ongezeko la asilimia 83.3, ikiwa ni wastani wa ongezeko la asilimia 16.3 kwa mwaka. Kwa kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2025 (Januari – Juni), thamani ya mali katika soko la bima iliongezeka kutoka shilingi trilioni 2.340 mwishoni mwa mwaka 2024 hadi kufikia shilingi trilioni 2.495 kufikia tarehe 30 Juni 2025, ikiwa ni ongezeko la asilimia 6.6.

4.4.2 Thamani ya Mitaji

Aidha, thamani ya mitaji katika soko la bima imeimarika kutoka shilingi bilioni 416.0 mwaka 2021 hadi kufikia shilingi bilioni 847.3 mwaka 2024, sawa na jumla ya ongezeko la asilimia 103.7, ikiwa ni wastani wa ongezeko la asilimia 26.3 kwa mwaka. Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2025, thamani ya mitaji katika soko la bima iliongezeka kutoka shilingi bilioni 906 mwaka 2024 hadi bilioni 993 kufikia Juni 30, 2025, ikiwa ni ongezeko la asilimia 9.5;

4.5 Uandikishaji wa ada za bima

Uandikishaji wa ada za bima katika soko la bima nchini umeongezeka kutoka shilingi bilioni 911.5 mwaka 2021 hadi kufikia shilingi trilioni 1.418 mwaka 2024, sawa na jumla ya ongezeko la asilimia 55.6 katika kipindi cha miaka minne, ikiwa ni wastani wa ongezeko la asilimia 11.7 kwa mwaka. Aidha, katika kipindi cha Januari hadi Juni 2025, uandikishaji wa ada za bima umefikia shilingi bilioni 831.8

4.6 Mchango wa Bima katika pato la Taifa

Mchango wa bima katika pato la Taifa umeongezeka kutoka asilimia 1.68 mwaka 2021 hadi kufikia asilimia 2.01 mwaka 2023 na unatarajiwa kuongezeka hadi kufikia asilimia 3 ifikapo mwaka 2030;

4.7 Bidhaa Mpya za Bima

Kuanzia mwaka 2021 hadi 2024, kumekuwa na ongezeko la bidhaa mpya za bima, ambapo kwa wastani bidhaa 15 mpya zimekuwa zikipewa idhini na Mamlaka kila mwaka kwa ajili ya kuuzwa katika soko la bima nchini. Katika kipindi cha Januari hadi Juni 2025, jumla ya bidhaa 10 mpya za bima zimepewa idhini na Mamlaka kuingia sokoni zikiwemo bidhaa za bima za kilimo na ufugaji;

4.8 Kiwango cha ubakizaji bima nchini

Kiwango cha ubakizaji bima nchini kwa Bima za Kawaida kimeongezeka kutoka asilimia 55.9 mwaka 2021 hadi asilimia 58.5 mwaka 2024. Aidha, kiwango cha ubakizaji bima kwa Bima za Maisha kimeongezeka pia kutoka asilimia 85.9 mwaka 2021 hadi kufikia asilimia 86.2 mwaka 2024;

4.9 Ulipaji wa Madai ya Bima

Ulipaji wa madai ya bima umeongezeka kutoka shilingi bilioni 397.6 mwaka 2021 hadi kufikia shilingi bilioni 592.1 mwaka 2024, sawa na jumla ya ongezeko la asilimia 48.9 katika kipindi cha miaka minne, ikiwa ni wastani wa ongezeko la asilimia 10.5 kwa mwaka. Aidha, wastani wa muda unaotumika na kampuni za bima kulipa madai ya bima yasiyo na utata umeimarika kutoka wastani wa siku 73 hadi ndani ya wastani wa siku 45; na

4.10 Mchango wa Sekta ya Bima kwenye mapato ya Serikali

Mchango wa Sekta ya bima kwenye mapato ya Serikali kupitia kodi mbalimbali ikiwemo Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na Kodi ya Kampuni (corporate tax) pekee umeongezeka kutoka shilingi bilioni 137.7 mwaka 2022 hadi kufikia shilingi bilioni 183.1 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 32.97.

5. MAENDELEO NA TAFITI KATIKA SOKO LA BIMA

Kupitia usimamizi thabiti na uongozi bora wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, sekta ya bima imepiga hatua kubwa katika eneo la maendeleo ya kitaasisi na kisera, pamoja na tafiti na ubunifu wa mifumo ya usimamizi wa soko la bima. Mwelekeo huu umewezesha mazingira bora ya uwekezaji, ushindani, na utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Mafanikio haya ni matokeo ya juhudi mahususi za Serikali kuweka misingi imara ya kitaasisi, kisheria na kiufundi inayowezesha ukuaji endelevu wa sekta ya bima nchini. Baadhi ya mafanikio haya ni pamoja na:

5.1 **Kuanzishwa kwa Konsotia za Bima ya Kilimo na Mafuta na Gesi:** Serikali imesimamia uanzishwaji wa Konsotia maalum za Bima katika maeneo ya kimkakati, ikiwa ni sehemu ya kuhakikisha ushirikiano wa sekta binafsi katika kutoa kinga ya bima kwenye maeneo yenye vihatarishi vikubwa. Konsotia ya Bima ya Kilimo imeundwa kwa kushirikisha kampuni kumi na tano (15) za bima, zinazotoa huduma kwa wakulima katika maeneo mbalimbali ya uzalishaji. Aidha, Konsotia ya Mafuta na Gesi imehusisha kampuni ishirini na mbili (22), ikiwa ni mkakati wa kulinda uwekezaji mkubwa katika sekta hiyo nyeti ya uchumi;

5.2 Kuandaa rasimu ya Andiko Dhana (Concept Paper) na Kanuni za Udhibiti wa Mazingira ya Majaribio ya Teknolojia, bidhaa au huduma za bima kabla ya kuingizwa sokoni (Regulations For Insurance Regulatory Sandbox);

5.3 Katika kuboresha ufanisi na uadilifu katika soko la bima, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bima imeandaa miongozo mbalimbali ya kisera na kiutendaji, ikiwemo:

5.3.1 Miongozo ya Kushughulikia Madai ya Bima;
5.3.2 Miongozo ya utawala bora;
5.3.3 Miongozo ya uondoaji wa kampuni za bima katika soko;
5.3.4 Miongozo ya Uanzishwaji wa kitengo cha Takwimu Bima katika kampuni;
5.3.5 Miongozo inayosimamia Bima ya Afya kwa Wote;
5.3.6 Miongozo ya Uwakala wa Ufuatiliaji wa Madai ya Bima;
5.3.7 Miongozo ya Viwango Elekezi vya Fidia ya Bima wa Madai ya Majeraha ya Mwili na Vifo kwa Mtu wa Tatu kutokana na Ajali za Barabarani;
5.3.8 Miongozo ya Usimamizi na Uondoaji wa Salveji;
5.3.9 Miongozo ya Usimamizi wa Vihatarishi na Mitaji;
5.3.10 Miongozo ya Benkibima (Uendeshaji wa Biashara);

5.3.11 Miongozo kuhusu utekelezaji wa viwango vya kimataifa vya taarifa ya kifedha inayohusu mikataba ya bima (IFRS 17);

5.3.12 Mwongozo wa utoaji huduma za bima kidijitali;

5.3.13 Mwongozo wa uendeshaji wa Takaful;

5.3.14 Miongozo ya Usimamizi wa Ubakizaji wa Bima na Bima Mtawanyo;

5.3.15 Miongozo ya Utoaji Idhibati kwa Warekebishaji na Watengenezaji wa Vyombo vya Moto Wanaohudumia Sekta ya Bima; na

5.3.16 Miongozo ya Bidhaa za Bima.

5.4 Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bima, imeendelea kufuatilia kwa karibu hatua za kukamilisha Sera ya Taifa ya Bima, pamoja na kuandaa Kanuni za Utekelezaji wa Bima za Lazima, hatua ambazo zitatoa mwongozo madhubuti wa namna ya kutekeleza bima ambazo ni za lazima kisheria, kwa lengo la kulinda wananchi na mali zao.; na

5.5 Serikali kupitia TIRA imeendelea kuimarisha ushirikiano na wadau wa maendeleo kama vile UNDP, GIZ, CRDB na wengineo, kwa ajili ya kutekeleza mikakati mbalimbali ya kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma za bima, kuimarisha elimu ya bima kwa jamii, na kusaidia katika maendeleo ya bidhaa mpya za bima zenye tija kwa wananchi.

6. MATUMIZI YA TEHAMA

Katika kutekeleza maono ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi madhubuti wa **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, juhudi kubwa zimefanyika katika kuimarisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ndani ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA). Mazingira mazuri ya kisera na kiutendaji yaliyowekwa na Serikali yameiwezesha Mamlaka kutumia TEHAMA kuboresha mifumo ya usimamizi wa soko la bima, kuongeza uwazi, kurahisisha huduma kwa wateja, na kuimarisha usalama wa taarifa.

Baadhi ya hatua mahususi zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:

6.1 Kufanya marejeo ya sera ya TEHAMA (ICT Policy), sera ya Usalama wa TEHAMA (ICT Security Policy) pamoja na Sera ya Matumizi Rasmi ya TEHAMA (ICT Acceptable Use Policy).

6.2 Kufanya marejeo ya mpango mkakati wa TEHAMA (ICT Strategy) na kuoanisha na marejeo yaliofanyika kwenye Mpango Mkakati wa Mamlaka (Cooperate Strategic Plan) kwa kipindi cha mwaka 2022/2023 – 2025/2026 ili kuhakikisha juhudi za TEHAMA zinaendana na dira ya Mamlaka.

6.3 Kusimamia vihatarishi na usalama wa TEHAMA ikiwemo kuridhia kushirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao (eGA) kufanya Tathmini ya mifumo ya kieletroniki inayotumiwa na Mamlaka katika kutekeleza shughuli zake na kutoa mapendekezo ya maboresho;

6.4 Kuboresha mifumo ya TEHAMA ambayo ni muhimu katika utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka ikiwemo mifumo ya:-

6.4.1 TIRAMIS – mfumo wa ufuatiliaji wa biashara za Bima nchini unaowawezesha watoa huduma ya Bima kuwasilisha taarifa za mauzo ya Bima kwa Mamlaka.

6.4.2 ORS - mfumo unaowezesha watoa huduma za bima kujisajili na kuhuisha leseni na taarifa zao;

6.4.3 TSS - mfumo unaowezesha Mamlaka kukusanya taarifa za mauzo ya Bima na kuchakata tozo ya Bima kila mwezi. Pia, mfumo unawezesha watoa huduma za bima ritani za mauzo ya Bima ya kila mwezi.;

6.4.4 IRIS – mfumo wa usimamizi wa utendaji wa watoa huduma za bima ambao kwa sasa upo katika hatua za matengenezo ili kuwa na mfumo thabiti wa usimamizi wa watoa huduma za bima.

6.5 Kuunganisha mifumo na Taasisi za Serikali ili kuwezesha utekelezaji wa Sheria ya Bima Sura ya 394 pamoja na kupata taarifa muhimu zinazotumika kwenye shughuli

za bima. Mifumo ya Taasisi iliyounganishwa na Mamlaka ni pamoja na NIDA, TRA, BOT, TPF, BRELA na LATRA;

6.6 Kuanzisha matumizi ya mfumo wa kuendesha vikao vya Bodi na Menejimenti (e-Board);

6.7 Kusimamia matumizi ya mifumo ya Kitaifa katika maeneo mbalimbali ya shughuli za Mamlaka ikiwemo mfumo wa Manunuzi ya Umma (NeST) na mfumo wa upimaji wa utendaji wa watumishi na Taasisi (PEPMIS/PIPMIS);

6.8 Kuimarisha utunzaji wa taarifa za Mamlaka katika Kituo cha Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA Data Centre) kwa lengo la kuhakikisha usalama wa taarifa, kudumisha upatikanaji wa Huduma za TEHAMA pamoja nakupunguza gharama.

7. ELIMU KWA UMMA

Kupitia uongozi madhubuti wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali imeendelea kuimarisha juhudi za utoaji wa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa bima katika maisha ya kila siku ya wananchi na maendeleo ya taifa. Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), kwa mwongozo wa Bodi, imefanikiwa kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuelimisha umma, kukuza uelewa wa masuala ya bima, na kuimarisha mahusiano kati ya Mamlaka na wadau wa sekta ya bima nchini.

Mafanikio hayo yanajumuisha:

7.1 **Kuanzisha miongozo na mikakati kwa ajili ya kuratibu shughuli za utoaji elimu** na mawasiliano kwa umma ikiwemo Mpango Mkakati wa Mawasiliano wa TIRA (TIRA Communication Strategy) na Mpango wa Taifa wa Utoaji Elimu ya Bima (National Insurance Education Strategy);

7.2 **Kuhamasisha Umma kuhusu dhana na umuhimu wa bima na kuimarisha mahusiano** kupitia mikutano ya wadau mkoa kwa mkoa ambapo warsha,

mikutano na semina zipatazo 206 kupitia Kanda mbalimbali zimefanyika, vipindi vya redio 56, vipindi vya runinga 44 na habari za kwenye magazeti 30. Aidha, Mamlaka imefanya jumla ya mikutano 6 na wahariri wa vyombo vya habari;

7.3 **Kuimarisha matumizi ya utumiaji wa vyombo mbalimbali vya habari** katika kutoa elimu kwa Umma ikiwemo matumizi ya mitandao ya kijamii (instagram, facebook, twitter) ambapo taarifa zipatazo 480 zilichapishwa na kuwafikia wafuasi zaidi ya 11,000;

7.4 **Kuanzisha ukurasa maalum wa makala kuhusu umuhimu wa bima kwa wananachi** kila mwezi. Aidha, Mamlaka imeanzisha jarida maalumu la bima ambalo linatoka kila mwezi;

7.5 **Kushiriki katika maonesho ya Kitaifa na Kimataifa** ikiwemo Maonesho ya Kimataifa ya Biashara (Saba Saba), Maonesho ya Wakulima (Nane Nane), Wiki ya Utumishi wa Umma, Wiki ya Madini, Wiki ya Fedha, Wiki ya Sheria, Maonesho ya Kimataifa ya Biashara Zanzibar, Maonesho ya Tamasha la Kizimkazi Zanzibar na Siku ya Wanawake Duniani. Kupitia matukio hayo Mamlaka imeendelea kufanya kampeni za umuhimu wa kuwa na bima na kutoa ushauri katika masuala ya bima;

7.6 **Kutoa michango ya kijamii (Corporate Social Responsibility)** katika sekta mbalimbali ikiwemo Afya, Elimu, Michezo, Ujenzi pamoja na maafa kwa lengo la kuimarisha mahusiano na jamii na kuboresha sekta ya bima;

7.7 **Ushirikiano na jumuiya ikiwemo mbalimbali za wanawake katika kuwasaidia** wanawake masuala ya kifedha na ulinzi katika bima mfano wa Jumuiya hizo ni kama TAWiFA na JUMAKITA; na

7.8 Kukutana na Wadau mbalimbali wa Mamlaka katika mikoa kwa lengo la kupata mrejesho wa huduma na kupokea maoni, ushauri na mapendezo kwa lengo la kuboresha huduma kwa wadau wa Bima.

8. USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU NA MASLAHI YA WATUMISHI

Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,** imeendelea kuimarisha usimamizi wa rasilimali watu kwa kuhakikisha watumishi wanatekeleza majukumu yao katika mazingira bora, wezeshi, na yenye kuzingatia maadili ya utumishi wa umma. Kupitia usimamizi thabiti wa Bodi ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), hatua mbalimbali zimechukuliwa katika kuboresha maslahi, kuongeza tija, na kuimarisha ustawi wa watumishi wa Mamlaka.

Hatua hizo ni pamoja na:

8.1 **Kujenga Jengo la Ofisi ya Makao Makuu ya Mamlaka Jijini Dodoma** ambapo ujenzi huo unatarajiwa kukamilika kabla ya mwezi Juni 2025. Kwa sasa jengo limekamilika kwa asilimia 80. Aidha, kufanya ukarabati wa Ofisi ya Mtendeni Dar Es Salaam na kuendelea na ukarabati wa Ofisi ya Zanzibar. Pia, kuhamisha Ofisi ya Kanda ya Mashariki kutoka Jengo la Wizara ya Mambo ya Ndani Makao Makuu kwenda Jengo la PSSSF Commercial Complex lililopo Barabara ya Sam Nujoma Ubungo DSM;

8.2 **Kuanzisha ofisi mpya za Kanda kutoka Ofisi 5 mwaka 2022 hadi kufikia ofisi kumi (10) mwaka 2024**. Lengo la kuanzisha Kanda hizi mpya ni kusogeza huduma kwa wananchi.

8.3 **Kuanzisha na kuhuisha Sera na Miongozo mbalimbali ya usimamizi** wa Rasilimaliwatu ikiwemo Muundo wa Maendeleo ya Utumishi, Kanuni za Utumishi wa TIRA, Mpango wa Motisha wa TIRA, Sera ya UKIMWI na magonjwa sugu yasiyoambukiza pamoja na Sera ya Utunzaji wa Nyaraka;

8.4 **Kutekeleza Mpango wa Mafunzo wa Mamlaka** wenye lengo la kuwajengea uwezo watumishi ili kumudu majukumu yao;

8.5 **Kuhuisha Muundo na Mgawanyo wa Majukumu wa Mamlaka** ili kuwezesha kuanzisha idara itakayosimamia utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote.

8.6 **Kusimamia utekelezaji wa majukumu ya watumishi kupitia mfumo wa e-Utendaji** unaojulikana kama '*Public Employees Performance Management Information System'* (PEPMIS); na

8.7 **Kuimarisha utawala bora** ambapo kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2025 jumla ya vikao sita (6) vya Baraza la Wafanyakazi vimefanyika.

9. USIMAMIZI WA FEDHA, MALI NA VIHATARISHI

Kutokana na uongozi hodari wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mamlaka imeendelea kuimarisha usimamizi wa fedha, mali na vihatarishi, na kufanikisha mafanikio makubwa kama ifuatavyo:

9.1 **Kupata Hati Safi za Hesabu** katika kipindi chote na kuhakikisha taarifa za Hesabu za Mamlaka zinawasilishwa kwa wakati kwa mujibu wa Sheria;

9.2 **Kuongeza mapato kutoka shilingi 18.04 bilioni mwaka 2022 hadi kufikia shilingi 24.64 billioni** mwaka 2024;

9.3 **Kutoa gawio kwa Serikali** kila mwaka ili kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa jumla ya kiasi cha **Shilingi 9.6 Bilioni kwa kipindi cha mwaka 2022 hadi 2024 kwa** mujibu wa Sheria; na

9.4 **Kuanzisha Sera ya Udhibiti Vihatarishi, Mfumo wa Udhibiti Vihatarishi, Sera ya Ufichuzi Taarifa za Siri, Sera ya Kuendeleza Shughuli za Mamlaka, na *Disaster Recovery Plan*** kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa vihatarishi na uendelevu wa shughuli za Mamlaka.

10. USIMAMIZI WA SHUGHULI ZA USULUHISHI WA MIGORORO

Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, hatua muhimu zimechukuliwa katika kuimarisha utatuzi wa migogoro ya bima, kwa lengo la kuhakikisha madai na malalamiko ya wananchi yanashughulikiwa kwa haki, haraka na kwa weledi. Baadhi ya mambo yaliyofanywa na Serikali katika Ofisi ya Msuluhishi wa Migogoro ya Bima (TIO) ni kama ifuatavyo:

10.1 Kupata Msuluhishi wa Migogoro ya Bima;

10.2 Kufanya marejeo ya Mpango Mkakati wa TIRA na kujumuisha shughuli za Msuluhishi wa Migogoro wa Bima (TIO);

10.3 Kujumuisha shughuli za mawasiliano za TIO kwenye Mpango Mkakati wa Mawasiliano wa Mamlaka (Communication Strategy);

10.4 Kuanza kuunda mfumo wa kielektroniki wa kushughulikia migogoro ya Bima ambao utaboresha utendaji wa TIO;

10.5 Kutambuliwa kwa nafasi ya Ofisi ya Msuluhishi wa Migororo ya Bima (TIO) katika Muundo na mgawanyo wa majukumu wa Mamlaka.

11. FURSA ZILIZOPO KWENYE SEKTA NDOGO YA BIMA

Sekta ndogo ya bima imeendelea kutoa fursa mbalimbali kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Fursa mahususi ni pamoja: -

i) Kukua kwa kasi ya maendeleo ya miundombinu na uanzishwaji wa viwanda, utalii na uchimbaji madini ambayo yanahitaji mikataba ya bima ili kupunguza Vihatarishi kwa wawekezaji na wale wenye mtaji mdogo wa urejeshaji;

ii) Ongezeko la watu na soko ambalo halijatumika hasa katika sekta isiyo rasmi;

iii) Uwepo wa teknolojia mpya na matumizi makubwa ya TEHAMA;

iv) Fursa katika Uwekezaji wa Biashara ya bima mtawanyo. Kwa sasa kuna Kampuni tatu (3) tu za bima mtawanyo;

v) Fursa za kuwekeza katika biashara ya Takaful;

vi) Fursa za kushiriki katika Konsotia za bima zilizoanzishwa ikiwa ni pamoja naKonsortia ya Mafuta na Gesi (Energy and Gas Co- insurance Consortium), na Konsotia ya Bima ya kilimo (Agriculture Insurance Consortium).

vii) Fursa katika Biashara za Bima ya Maisha ambayo inaendelea kukua hapa Tanzania;

viii) Kupanua wigo wa bima ya lazima ili kujumuisha bidhaa zinazoagizwa kutoka nje, masoko ya umma, majengo ya biashara, vyombo vya baharini, feri, na mashua;

ix) Uanzishwaji wa bodi ya wataalam wa Bima, Hifadhi ya Jamii na Takwimu Bima utaongeza na kuchochea uwepo wa rasilimaliwatu katika sekta ndogo ya bima; na

x) Kuongezeka kwa programu za elimu na uhamasishaji wa umma kuhusu matumizi ya bima kunatarajiwa kuongeza mahitaji ya bidhaa za bima.

12. CHANGAMOTO NA HATUA ZA UTATUZI

Sekta ndogo ya bima inakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwemo kukosekana kwa sera ya taifa ya bima; kukosekana kwa mpango wa Taifa wa bima nafuu za kilimo; utumiaji mdogo wa bima; na upatikanaji duni wa bidhaa na huduma za bima. Mamlaka kwa kushirikiana na wadau wengine imeendelea kutekeleza hatua za kukabiliana na changamoto husika kama ifuatavyo:-

Jedwali Na. 3: Changamoto Soko la Bima na Hatua za Utatuzi

Na.	Changamoto	Hatua za Utatuzi
1.	Kukosekana kwa Sera ya Bima ya Taifa	Mamlaka inaendelea kuishirikisha Wizara ya Fedha kukamilisha mchakato wa Sera ya Bima ya Taifa. Sera inasubiria mapitio na mamlaka za juu za serikali.

Na.	Changamoto	Hatua za Utatuzi
2.	Kukosekana kwa Skimu ya Taifa ya Bima za Kilimo	Kuendelea kushirikisha Wizara za kisekta (ikiwa ni pamoja na Wizara ya Fedha, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wadau wa maendeleo na wadau wengine muhimu wa sekta ndogo ya bima kuanzisha Skimu ya Taifa ya Bima za Kilimo.
3.	Kutokuwepo kwa Kanuni za Bima ya Lazima	TIRA imeendelea kuishirikisha Wizara ya Fedha kuhakikisha rasimu ya Kanuni za Bima za Lazima inakamilika na Kusainiwa na Waziri wa Fedha.

13. MIPANGO TARAJIWA YA MAMLAKA, 2025/26 – 2026/27

Mamlaka inatarajia Soko litafikia makisio ya ukuaji wa angalau asilimia 15 katika kipindi cha 2025/26 – 2026/27. Aidha,Sekta ndogo ya bima inatarajiwa kubaki thabiti kifedha katika siku zijazo. Vipaumbele vya vya sekta ni pamoja na vifuatavyo:-

i. Kukamilisha Sera ya Taifa ya Bima na mkakati wake wa utekelezaji;

ii. Kuanza rasmi kwa usimamizi wa mfumo wa Bima ya Afya kwa wote kwa mujibu wa Sheria, Taratibu na Kanuni husika;

iii. Kukamilisha ujenzi wa mifumo mipya ya TEHAMA kwa ajili ya usimamizi wa Bima ya Afya kwa Wote (UHI) ikiwa ni pamoja na Mfumo Jumuishi wa Udhibiti wa Bima (Insurance Regulatory Integrated System – IRIS);

iv. Kukamilisha majadiliano ya Mikataba ya Uenyeji wa Tanzania Kwa ofisi za kampuni za Africa Reinsurance Corporation (AFRICA RE) na PTA Reinsurance Company (ZEP-RE);

v. Kukamilisha Marekebisho ya Sheria ya Bima SURA 394;

vi. Kukamilisha Kanuni za Bima za Lazima;

vii. Kukamilisha taratibu za kisheria za uanzishaji wa Skimu ya Taifa ya Bima za Kilimo (ukamilishaji wa kanuni za Bima ya Kilimo);

viii. Kuandaa Mpango Mkakati Mpya wa Mamlaka wa Kipindi cha Miaka 5 ijayo 2026/27 – 2030/31 ambao pamoja na mengine utaainisha mikakati mipya ya uendelezaji wa sekta ndogo ya bima kwa kuzingatia mipango ya kitaifa ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 na Ilani ya CCM 2025-2030;

ix. Kuimarisha ushirikiano na washirika wa maendeleo wa kimkakati;

x. Kukamilisha na kutekeleza Mfumo wa Udhibiti wa mazingira ya majaribio kwa bidhaa na huduma mpya za bima (Insurance Sandbox Regulatory Framewok) na Kanuni zake; na

Kukamilisha uunganishaji wa mfumo wa TEHAMA wa TIRA na mifumo ya TEHAMA ya taasisi zingine za umma (Jeshi la Polisi, LATRA, NIDA, TASAC, TRA, ZRA) kwa lengo la kuimarisha usimamizi na maendeleo ya sekta ndogo ya bima nchini.

14. SHUKRANI KWA WAHARIRI NA WAANDISHI WA HABARI

Mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya bima katika kipindi cha miaka minne iliyopita, yamechangiwa Serikali ya awamu ya Sita chini Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan Rais wa JMT kutokana na sera na mazingira rafiki ya ufanyaji biashara nchini ikiwemo Soko la Bima. Aidha, niwapongeze sana waandishi, wahariri na vyombo vya habari kwa kazi kubwa ya kutoa elimu kwa Umma ikwemo umuhimu wa bima kwa wananchi.

Mamlaka inawashukuru kwa nafasi hiyo ya kipekee na inawahimiza waendelee kushirikiana nasi katika kutoa elimu kwa wananchi kupitia makala, taarifa, mijadala na vipindi vya elimu. Kupitia uandishi na uchambuzi wenu, mmeonesha mambo muhimu yanayofanywa katika sekta ya bima na hivyo kuongeza uelewa wa jamii kuhusu umuhimu wa bima katika maisha na uchumi wa taifa. Mamlaka ipo tayari kuendeleza ushirikiano nanyi ili kuimarisha zaidi maendeleo ya sekta ya bima nchini.

15. HITIMISHO

Sekta ya bima nchini imeendelea kukua kwa kasi na kuimarika kwa viwango vya kuridhisha, ikiwa ni matokeo ya juhudi thabiti, sera sahihi na mwelekeo wa kimkakati uliowekwa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu**.

Kupitia maelekezo na msukumo wa Mheshimiwa Rais, Serikali imewezesha maboresho makubwa katika mifumo ya usimamizi wa sekta ya bima, uanzishwaji wa sheria, kanuni na miongozo muhimu, upanuzi wa huduma kwa wananchi, pamoja na uimarishaji wa taasisi zinazosimamia sekta hiyo. Hatua hizi zimejenga msingi imara wa sekta ya bima shindani, jumuishi na inayochangia kikamilifu katika kulinda maisha, mali na ustawi wa wananchi pamoja na uchumi wa taifa kwa ujumla.

Kwa msingi huo, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) itaendelea kushirikiana na Serikali, wadau wa maendeleo na sekta binafsi katika kuhakikisha sekta ya bima inazidi kuimarika, kupanua wigo wa huduma na kuchangia kwa kiwango kikubwa katika ajenda ya maendeleo ya taifa letu.